


MUUNDO WA INJILI YA UKWELI NA NYRON MEDINA



Watu wengi wanakosa kujua kile kiini cha injili, wanakosa kujua kwa kifupi, ni nini kwa mukhtasari **sayansi** ilio katika ndani ya injili inayofanya injili kuitwa injili, na ni nini hasa kinachoipatia injili nguvu ya kuokoa wanadamu kutoka kwenye dhambi. Lakini Paulo anatuambia kwamba "...kwa maana siionei haya injili, kwa sababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu, kwa kila aaminie, kwa myahudi kwanza, na kwa myunani pia ..." **warumi 1:16**; na ni nini kinachoipatia injili huu "uwezo" (Greek "**dunamis**", inayomaanisha "**namna inavyo fanya kazi**") wa kuokoa wanadamu? Paulo anatuambia kwamba "Haki ya Mungu" ilio ndani ya injili "kupitia kwa imani" ndiyo inayofanya injili kuweza **kufanya kazi** ya kuokoa wenye dhambi (**Warumi 1:17**).

Hata hivyo, watu wengi wanafikiria kwamba "haki ya Mungu" ni ile sheria ya **Amri kumi** tu. Ni kweli kwamba hiyo haki ya Mungu ni hizo Amri za Mungu, kwa sababu tunaambiwa kwamba "amri zako zote ni haki" **Zaburi 119:172**, na Paulo anatuambia kwamba "... hayo maagizo (haki) ya sheria yaweze kutimizwa ndani yetu ..." **Warumi 8:4**. Lakini tunaambiwa kuhusu haki nyingine; **Haki ya Mungu** ambayo ni **bila** hiyo sheria ya Mungu, au "tofauti na" matendo ya sheria. "... kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria. Lakini sasa, haki ya Mungu pasipo [tofauti na] hiyo sheria imedhihirishwa, inashuhudiwa na torati [vitabu vitano vya Musa alivyoandika] na manabii." **Warumi 3:20,21**.

Tunachoelezwa katika vifungu hivi na Paulo ni Kwamba, wakati hio **sheria ya Amri kumi** inatuelimisha kuhusu dhambi, kuna **Haki ya Mungu** ambayo ni tofauti na torati ya Mungu, au tofauti na hayo **matendo** ya sheria ya amri kumi.

Hi **haki ya Mungu inashuhudiwa** pia na **kupatikana** katika maandiko ya Musa (torati) na pia inapatikana katika maandiko ya manabii. Mfano ulio wazi na uelezao kuhusu jambo hili la "**Haki ya Mungu**" kwenye maandiko ni; "Tazama siku zinakuja, asema BWANA, nitakapomchipushia Daudi tawi la haki, na Mfalme ata tawala na kufanikiwa ... Katika siku zake Yudah ataokolewa ... na hili ndilo jina ambalo kwa hilo ataitwa, BWANA HAKI YETU." **Yeremia 23:5,6**. Andiko hili latwambia kwa uwazi kwamba huyo BWANA, YHWH kutoka awali, (inayoandikwa Yawe), ndiye **Haki** yetu. Mungu si sheria Yake ya matendo, kwa hivyo hio Haki ya Mungu ambayo ni **tofauti** na matendo ya torati, ni **Mungu Mwenyewe**, ili kwamba YAWE Haki yetu ni **YAWE Mwenyewe**. (Tazama: **Zaburi 7:17; Zaburi 143:11**).

Sasa kuhusu hii **Haki ya Mungu** ambayo ni **Mungu Mwenyewe**, tunaambiwa kwa undani zaidi namna ambayo huo **mpango wa wokovu** unavyo fanya kazi: "Hata haki ya Mungu ijayo kwa imani ya Yesu Kristo kwa [Maandishi ya Kigiriki yanasema "eis" inayomaanisha "ndani ya"] wote waaminio. Maana hakuna tofauti."

Warumi 3:22. Kwa hivyo Andiko hili latwambia kwamba hio **Haki ya Mungu, Mungu Mwenyewe**, anakuja **ndani yetu** kwa njia ya Imani ya Yesu Kristo. Hio **Haki ya Mungu, Mungu Mwenyewe**, anakuja kukaa ndani yetu; **mionyi** mwetu kulengana na **Zaburi 40:10**. Hivi ni sawa na kusema **Mungu anakaa ndani yetu** kupitia kwa **Roho Mtakatifu**. **1Yohana 4:12,13**. Ni wakati ambapo **Mungu**, kama **Haki ya Mungu** anapokuja kukaa ndani yetu kupitia kwa Imani ndipo **tunapofanywa kuwa haki, ndipo** tunawezeshwa **kutunza** sheria ya Mungu, au hio **haki ya sheria** ina thibitishwa ndani yetu kulengana na **Warumi 3:28,30,31** na **Warumi 8:4**.

Kwa hivyo hiki ndicho **kiini** cha injili kwa ufupi kinachoifanya injili ikuwe Injili halisi iokoayo: Hio Haki ya Mungu, Mungu Mwenyewe, lazima aje akae moyoni kupitia kwa Imani, ili hii Imani ya Kristo na Mungu Mwenyewe ata tuhamasisha kufanya matendo au haki hio ya sheria. Huu ndio ujumbe wa 1 Yohana 3:24, na hivi pekeake ndivyo vinawenza kumpa Mungu utukufu halisi. Wakati matendo ya kutunza sheria tunayatenda kutokana na kuhamasisha na Mungu Mwenyewe (Haki ya Mungu) akaaye ndani yetu, Mungu pekee atatukuzwa kati yetu. Hivyo basi hiki ndicho **kiini halisi cha injili**, ambapo, wakati mtu anacho katika falsafa yake, anayo **Injili halisi**. Amina.